# SIRI YA UTII



JAMES KALEKWA

# SIRI
# YA
# UTII

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Dokezo la Utii..........................................................................3

Ngazi nne za Utii...................................................................... 5

Kina cha Utii:......................................................................... 18

Thawabu ya Utii......................................................................21

Kuhusu Mwandishi:...................................................................24

Kuhusu New Vine Church...........................................................24

Mawasiliano na Mwandishi:.......................................................25

# Dokezo la Utii

*"Naye Samweli akasema, Je! BWANA huzipenda sadaka za kutekeketezwa na dhabihu sawasawa* ***na kutii sauti ya BWANA?*** *Angalia, k****utii ni bora kuliko dhabihu,*** *Na kusikia kuliko mafuta ya bebeeru."* 1 Samweli 15:22

Ukimuwekea Mungu machaguo mawili ili achague mojawapo kati ya hayo; upande mmoja uweke sadaka na upande mwingine uweke utii. Uwe na uhakika Mungu huchagua utii. Hata hivyo, ni heri ukijua ya kwamba sadaka ni udhihirisho wa utii wetu kwa BWANA. Sadaka yoyote inayowasilishwa nje ya kigezo cha utii, Mungu huiona kama "hela" tu! Haisemi chochote mbele zake.

Kama utii ni muhimu kiasi cha mvutia Mungu hivyo, utii ni nini basi?

- Utii ni kukubali na kutendea kazi maelekezo ya Mungu bila kuyatilia mashaka.

- Namna tunavyohusiana na Mungu na kumwendea ni kwa utii. Hii ni kwa sababu kwenye mahusiano hayo, Mungu hutoa maelekezo na si mapendekezo. Mapendekezo hupokelewa kwa majadiliano. Wakati maelekezo hupokelewa kwa utii tu na si pungufu ya hapo.
- Neno na maelekezo ya Mungu hupokelewa kwa utii na si kwa uchaguzi. *"Neno la Mungu ni kwa ajili ya utekelezaji na si uchambuzi."* Dr. Sam Adeyemi
- Upendeleo ya kiungu uko ng'ambo ya pili ya barabara ya utii unakusubiri. Je, utavuka?

# Ngazi nne za Utii:

1. **Utii kuyaelekea maandiko matakatifu (Biblia).**

*"2. Katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, mimi Danieli, kwa kuvisoma vitabu, nalifahamu hesabu ya miaka, ambayo eno la BWANA lilimjia Yeremia nabii, ya kuutimiza ukiwa wa Yerusalemu, yaani, miaka sabini. 3. Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga, na kuvaa nguo za magunia na majivu,"* **Danieli 9:2-3**

Kile alichokisoma Danieli kinapatikana kwenye vitabu vifuatavyo: Yeremia 25:11-12; 29:10; Ezra 1:1; 2 Nyakati 36:21. Angeweza kusoma kama machapisho tu au vitabu vya historia ya taifa lake au masimulizi kutoka kwa waandishi wazuri na wema wa taifa lake zuri la Israeli. Lakini aliuvuka huo mtego. Aliposoma, alichukua kile alichokisoma kwa uzito na heshima ya hali ya juu sana. Alijua ya kwamba anachokisoma ni **neno la BWANA**.

Mwitikio wake juu ya kile alichokisoma unatuambia hali nya moyo wake kuyaelekea maandiko matakatifu, "…*Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka kwa maombi…*". Hii ni heshima na mwitikio wa hali ya juu sana kwa neno la Mungu. Halikuwa neno lililoishia kumpa taarifa tu, bali liliyakunja magoti yake.

Hakuna mahali kwenye unabii huo ambapo Danieli alitajwa kwa jina ya kwamba ana wajibu wa kuomba au kutenda chochote ili litokee na kuwa halisi kwenye maisha ya watu wake. Kilichoyakunja magoti yake, ni hali ya utii uliokuwa ndani yake kuliekea neno la Mungu.

Iko hivi, kila ukisoma maandiko matakatifu ukagundua yanamuhusu kila mmoja isipokuwa wewe, ujue kuna upungufu wa utii ndani yako kuyaelekea maandiko.

Kabla haujaanza kutafuta kusikia sauti ya Roho Mtakatifu, hakikisha umemaliza kuisikia iliyomo ndani ya neno lake; na kama unapenda sana unabii,

hakikisha umeupokea unabii wako wote tena uliokwisha kutimilizwa uliomo ndani ya maandiko matakatifu.

**2. Neno la Mungu lililovuviwa**

*"31. Tena kwa habari ya kiyama ya watu, hamjalisoma* ***neno lililonenwa na Mungu****, kusema, 32.* ***"Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka , na Mungu wa Yakobo?*** *Mungu si Mungu wa wafu bali wa walio hai."* Mathayo 22:31-32 (SUV). Ukisoma andiko hilo kutokea tafsiri ya NENO utagundua kuna msisitizo tofauti, "Lakini kuhusu ufufuo wa wafu, hamkusoma **kile Mungu alichowaambia**, kwamba," Utaona si tu kwamba Mungu alisema ujumbe ukaenda hewani, bali alikuwa anasema na hawa ndugu waliokuwa wanaongea na Bwana Yesu. Tafsiri nyingi za lugha ya kiingereza zinakubaliana kabisa na wazo hili ya kwamba si tu Mungu alisema ujumbe bali alisema na watu hawa huu ujumbe.

"But about the resurrection of the dead – have you not read **what God said to you,**" (NIV)

“But as touching the resurrection of the dead, have ye not read **that which was spoken unto you** by God saying,” (ASV)

“And as for whether the dead are resurrected, haven’t you read **what God said to you**,” (CJB)

Kwa msingi huo basi, twaweza kufikia hitimisho ya kwamba ndani ya neno la Mungu lililoandikwa kulikuwa na ujumbe ulimwendea Musa kama msikiaji wa awali. Hata hivyo halikuishia hapo, bali limebeba pumzi ya kukihudumia na kukifaa kizazi kilichokuwa kimesimama mbele ya Yesu… na halikuishia hapo, linasema hata hivi leo.

Kwa hiyo, unaposoma maandiko matakatifu, kumbuka kuizingatia pumzi na sauti iliyo nyuma na maandiko hayo. Utagundua ya kwamba maandiko waliyoandikiwa Wakorintho, Wathesalonike, Wagalatia, Waebrania na wengineo yanakufaa wewe mtanzania (na mtu mwingine yeyote) hivi leo!

*“Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena*

*lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."* **Waebrania 4:12**

Kila wakati unapofungua maandiko matakatifu kuyasoma, huwa yamefunuka kukusoma wewe. Huo ni uthibitisho wa pumzi iliyomo ndani ya neno. Usisome maandiko kama kitabu cha historia, bali ni pumzi hai ya Mungu hata hivi leo!

3. Maongozi ya Roho Mtakatifu

*"Kwa kuwa wote **wanaoongozwa na Roho wa Mungu**, hao ndio wana wa Mungu."* Warumi 8:14

"Lakini **mkiongozwa na Roho**, hampo chini ya sheria." Wagalatia 5:18

*"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, **atawaongoza awatie kwenye kweli yote**; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake."* Yohana 16:13

Nimekusudia uone ya kwamba moja wapo ya kiashairia cha uana wa Mungu ni kuongozwa na Roho wa Mungua ambaye ameachiliwa kwa ajili hiyo.

Kumbuka neno linamtambulisha Roho Mtakatifu kama msaidizi na si mlazimishaji. Kwa hiyo, namna yake ya kuongoza ni ile ya kutusaidia kuliko kutulazimisha zaidi. Nafasi hii ya "msaidizi" ndiyo mtego wenyewe. Unahitajika utii wa hali ya juu sana ili kuongozwa na msaidizi!

4. Mamlaka halali juu yangu:

Katika kuyaongoza na kuyaratibu maisha ya mwanadamu hapa duniani, Mungu ameyaweka chini ya mamlaka. Kuna mamlaka nyingi ambazo ziko juu ya maisha yako. Hata hivyo, kwa minajiri ya kitabu, ninatambulisha kwako mamlaka nne ambazo unapaswa kuzitii.

a) *Wazazi wa kimwili:* Hawa si tu kwamba ni watu waliokuleta duniani na kukupatia utambulisho wa kibaiolojia/vinasaba na kukupa ukoo. Hawa ni mamlaka! Tazama ni

kwa namna gani maandiko yamewaambatanisha na aina fulani ya uheri.

"Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote; maana jambo hili lapendeza katika Bwana." Wakolosai 3:21

"Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki 2. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, 3. Upate heri, ukae siku nyingi katika dunia." Waefeso 6:13

Kutotii mamlaka hii ya wazazi wa kibaiolojia ni kuchagua kutopokea thawabu iliyoambatanishwa pamoja nao.

*b) Wazazi wa kiroho*

"Kwa kuwa nakuamini kutii kwako ndiyo maana nimekuandikia, nikijua ya kuwa utafanya zaidi ya hayo nisemayo." Filemoni 1:21

Moja ya mifano ya mahusiano ya mzazi wa kiroho na mtoto wake na swala la utii ni katika ya mtume Paulo kama baba kwa upande mmoja; na Filemoni kama mwana kwa upande wa pili.

Kwenye waraka huu wenye sura moja, utaona malekezo ya baba kwa mwanae:

- Kumpokea Onesimo kama ndugu yake katika Kristo. Hapo awali Onesimo alikuwa ni mtumwa wa Filemoni na inaonekana aliotoroka na aliiba sehemu ya mali ya bwana wake (Filemoni 1:16)
- Kufuta madeni yote ya mali yaliyopita juu ya Onesimo. Lakini ikiwa ni muhimu sana kuendelea kuyadai, basi amdai baba yake, yaani mtume Paulo (Filemoni 1:18)
- Amuandalie baba yake mahali pa kukaa ambapo atafikia baada tu ya kumaliza kifungo chake gerezani (Filemoni 1:22)
- Tahadhari: Filemoni anakumbushwa na baba yake ya kwamba yeye anadaiwa nafsi

yake kabisa, siyo hata fedha au mali. Hii ni kwa sababu ya uwekezaji wa kiroho wa Paulo kwa mwanae (Filemoni 1:19b)

Sasa, ni vizuri uelewe ya kwamba ujasiri wa kutoa malekezo alionao Paulo kwa mwanae Filemoni ni kwa sababu ya kiwango cha utii wake si tu kwa sababu ya mamlaka ya kiroho ya Paulo.

*“**Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea;** maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi.”* Waebrania 13:17

Mwitikio wetu kwa wanaotuongoza ni utii na unyenyekevu. Kwenye andiko hili, wanaoongoza ni wale wanaokesha kwa ajili ya roho zetu na wenye wajibu wa kutoa hesabu juu ya maisha yetu. Ni nani mwingine afanye hivyo ispokuwa mzazi wako wa kiroho? Unadhani kuna mtu mahali fulani anaweza kukesha kwa ajili yako? Unadhani kuna mtu mahali fulani anaweza kujiweka kwenye jukumu la kuja kutoa

heshabu kwa ajili yako? Ni kwa nini ajiingine kwenye majukumu mazito hivyo?

c) Mume

Mume ni mamlaka kwa mke wake! Kama mke atatambua hivyo, atachukua neno la Mungu kama lilivyo na atatekeleza neno basi atavuna thawabu ya kutii kwake. Maandiko yanasema hivi kuhusu mamlaka hii.

*"22. Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. 23. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili 24. Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo."* Waefeso 5:22-24

Kwenye kitabu kiitwacho NYWILA nimefundisha kwa upana wake sana msukumo wa kiungu nyuma ya utii wa mwanamke kumuelekea mumewe. Mwanamke ameaminiwa Mungu kumfundisha mume wake utii kwa kuwa kilelezo cha huo utii wenyewe. Na mume, ambaye ni sehemu ya kanisa la Kristo, atatenda

inavyotarajiwa awapo kwenye nafasi yake ya bibi arusi wa Kristo.

Hata hivyo, ni vizuri kujua ya kwamba Mungu ndiye aliyeweka mtiririko huo wa kimamlaka si kwa ajili ya hasara au kutuonea bali ni kwa faida na ustawi wetu. Hili ni jambo ambalo linabishaniwa sana miongoni mwa tamaduni na mapokeo kiasi kwamba mtu anayeamini katika njia hii anaonekana kuwa ni wa kizamani na amepitwa na wakati. Atukuzwe Mungu kwamba vitu vyote vitapita, neno litasimama!

*"Ninyi wake, watiini waume zenu, kama ipendezavyo katika Bwana."* Wakolosai 3:18

*"Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi. Ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno."* 1 Petro 3:1

d) Kiongozi wa kazi

Kuelewa muktadha kidogo, ni kwamba wakati wa kanisa la mwanzoni kulikuwa kuna uatamaduni wa utumwa kwenye jamii za wakati huo. Lilikuwa ni

jambo la kawaida kabisa. Ikafikia wakati ambapo watumwa wanaiamini injili na wanaokoka··· wanfunguliwa kutoka katika **utumwa wa dhambi** (siyo utumwa wa kazi). Wengine walianza kuhoji ya kwamba, maadamu wamewekwa huru na Kristo kuna umuhimu gani tena wakuendelea kuwa chini ya utumwa wa bwana zao? Sasa ikumbukwe ya kwamba utumwa ndiyo ulikuwa mfumo wa kiuchumia wa uzalishaji (means of production) – ni kama ilivyo ajira kwa zama zetu. Kulikuwa na utaratibu na miongozo ya namna ya kukombolewa (kulipiwa deni au kujilipia deni la kutoka utumwani) au kuachilia huru kwa utashi wa bwana. Tofauti na hapo ilionekana kuwa ni uasi na athari zake zingekuwa kubwa.

Maandiko yanaelekeza ya kwamba watumwa wawaone bwana zao kama mamlaka ambayo hata kama umeokoka unapaswa kuiitikia kwa utii.

*“Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali*

*kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana."* Wakolosai 3:22

*"Enyi watumishi, watiini bwana zenu kwa hofu nyingi, sio walio wema na wenye upole tu, bali nao walio wakali."* 1 Petro 2:18

Ni sawa na zama hizi baada tu ya kuokoka usemi ya kwamba hupendi kuwa chini ya mtu, hupendi maelekezo yake, hupendi kubanwa… unataka umtii Kristo tu na neno lake! Hiyo siyo sawasawa. Ukiokoka, hakikisha viongozi wako wanauona mwenendo wako mwema kiasi cha kuwavuta kwa Yesu Kristo.

# Kina cha Utii:

1. **Ibrahimu:** Unapozungumzia swala la utii, moja ya vielelezo ni baba yetu wa Imani, Ibrahimu. Mungu alipomwita kutoka Harani kwenda kwenye nchi asiyoijua ambayo Mungu atamuonyesha huko mbele ya safari (Soma Mwanzo 12). Huwa ninajaribu kukaa kwenye nafasi ya Ibrahimu na kubakia kumshangaa tu. Fikiria unaenda kwenye stendi ya mabasi kupanda basin a hujui unashukia wapi? Ni mpaka uatakaposikia, "Shuka, ni hapa!" Inaeleweka hiyo?

   Lakini mwitikio wa Ibrahimu kwenye maelekezo ya Mungu *"Basi Abramu akaenda, kama BWANA alivyomwamuru….."* Mwanzo 12:4

   Unakumbuka kisa cha Ibrahimu kumtoa Isaka, mwanawe wa pekee kuwa sadaka ya kuteketezwa (Mwanzo 22)? Si jambo rahisi

kuelewa na hasa unapoona mwitikio wa Ibrahimu kwenye jambo hili, *"Ibrahimu akaondoka alfajiri…"* Mwanzo 22:3

Utii ulienda kwenye kina ambacho Mungu akisema chochote asiwe na mashaka, atakipata kwa mwitikio wa heshima kubwa kutoka Ibrahimu.

2. **Mashujaa wa Daudi:** Kuna kundi lililomzunguka Mfalme Daudi linafahamika kama mashujaa wa Daudi. Hawa ni sehemu ya wale waliomwendea kwenye pango la Adulamu wakiwa na dhiki, madeni na kuchoka. Wakati mmoja kiongozi wao alitamani maji toka kwenye kisima kilichozungukwa na majeshi mengi. Hata hivyo, wao walichagua kusikia tamanio la kiongozi wao kama amri. Waliitikia kwa kuchukua hatua za utekelezaji tu. Lilikuwa ni jambo hatari sana walifanya, na hicho ndicho kina chao cha utii.

*“Basi hao mashujaa watatu wakapenya jeshi la Wafilisti, wakateka maji kutoka kile kisima cha Bethlehemu, kilicho karibu na lango, wakayachukua, wakamletea Daudi; walakini yeye hakukubali kuyanywa, akayamimina mbele za BWANA. 17. Akasema, Hasha, BWANA, nisifanye hivi; je! Si damu hii ya watu hao waliohatarisha nafsi zao? Kwa hiyo hakukubali kuyanywa. Hayo ndiyo waliyoyafanya wale mashujaa watatu.”* 2 Samweli 23:16

Umewahi kumsikia mchungaji wako anatamani jambo fulani litokee kanisani? Huwa unaitikiaje?

3. Yesu Kristo: Bwana wetu Yesu Kristo alionyesha kielelezo cha utii. Alikuwa atii agizo na maelekezo ya baba yake.

*“tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.”* Wafilipi 2:8

# Thawabu ya Utii

1. Mema ya nchi –

*"Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi."*

Isaya 1:19. Mema ya nchi si chakula cha kila mtu bali kimetunzwa ajili ya watu waliotayari kukubali na kutii. Unataka kula mema yanchi? Karibu mezani… hakikisha unakuja na kuponi yako ya "kukubali na kutaa". Usisahau anayegawa thaabu hii ni Mungu mwenyewe, kwa hiyo hakuna namna utamfanyia ulaghai au udanganyifu.

2. Kuhudumia watu wengi: Kinsingi hapa nimekusudia uone utii unavyokufungulia mlango wa kuathiri maisha ya watu wengi. Hata hivyo, mkazo wangu hauko kwenye kuwa mtu maarufu tu, bali maisha yako au kile ulichokibeba kuhudumia maisha ya wengi (influence).

*"…wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzivunja muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa,*

*ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa."* Ufunuo wa Yohana 5:9b

Yesu alipokuwa duniani kabla ya kwenda msalabani alikuwa na kundi la watu wachache ndani ya nchi moja tu. Lakini baada ya kutii na kwenda msalabani aliupata ulimwengu wote kwa wakati mmoja. Inawezekana kama angebaki duniani na kutaka kumfikia mtu mmoja mmoja kwa mafundisho yake, angekuwa bado hajafika kwetu. Utii ulilipua uwezo wa huduma yake kufikia watu wengi

3. Jina kubwa: Ni vyema sana ukfahamu ya kwamba Mungu haimsumbui wala hapati tabu kulikuza jina lako. Ndivyo alivymuahidi mzee wetu Ibrahimu. Kwa sababu jina lake liko juu ya majina yote, haijalishi lako litakua kiasi gani litabaki chini ya jina lake. Hivyo yuko sawa tu!

*"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina."* Wafilipi 2:9

4. Kuingia kwenye orodha ya mashujaa wa imani

*"Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi."* Waebrania 11:40

Umegundua ya kwamba orodha ya mashujaa wa imani walio kwenye sura yote ya 11 ya Waebrania haijafungwa? Wao wametuwekea sisi kilelezo na sisi tunapaswa kutembea kwenye hicho kielelezo. Wao ni kama mchoro na sisi ni jengo la huo mchoro.

Ni vyema ujue, mlango alioingilia kwenye sura ya 11 ni Imani; na utii ni kionjo muhimu kujenga imani! Kuepuka utii, ni kuepuka imani. Na kuepuka imani ni kufunga mlango wa kuingilia kwenye mlango wa jumba la mashujaa wa imani.

Nimekuombea kwa BWANA YESU ya kwamba kiwango chako cha utii kitaongezeka kwa jina la Yesu Kristo. Kama Mungu anatafuta mtu atakayemtii na kuitikia sauti yake, akupate wewe

Iwe Amani, utele na utoshelevu kwako!

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764